Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili ab initio – Standard level – Paper 1
# Swahili ab initio – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili ab initio – Nivel medio – Prueba 1

Wednesday 4 May 2016 (afternoon)
Mercredi 4 mai 2016 (après-midi)
Miércoles 4 de mayo de 2016 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N’ouvrez pas ce livret avant d’y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

2216 – 2835



© International Baccalaureate Organization 2016

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

**Matini A**

# Leso yasaidia kufundisha Kiswahili

Leso ni nguo yenye maandishi ambayo yanalenga kutoa mafundisho kwa jamii, kupinga jambo baya kutokea katika jamii, kupongeza mambo mema na kuhimiza yaendelezwe katika jamii. Nguo hii mara nyingi huvaliwa na wanawake na hufungwa kiunoni na mara nyingine huvaliwa kutoka kichwani hadi mabegani kama mtandio. Vazi la leso huhusishwa na utamaduni wa watu wa pwani hasa pwani ya Afrika Mashariki na Visiwa vya Ngazija (Comoro).

**Mapambo**

Leso mara nyingi huwekwa mapambo nchini Kenya na Tanzania. Hata hivyo, leso huuzwa katika maeneo mengi huko bara na mengine huchuuzwa masokoni. Leso pia huuzwa katika mataifa ya ulaya. Watalii ambao huzuru maeneo ya mwambao wa pwani au bara hupenda kununua leso zenye maandishi ya Kiswahili kwa nia ya kutaka kujifunza maneno ya kimsingi ya Kiswahili.

Wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki hutembeza watalii katika masoko ili wanunue leso. Wenyeji pia huchukua jukumu la kutafsiri maandishi yaliyoandikwa katika leso kwa watalii hawa. Baadhi ya maandishi yanayopatikana katika leso ni: "Karibu Kenya, hakuna matata", "Urembo wa wanamke ni tabia, si sura", "Asante mama kwa malezi yako bora" na kadhalika. Kwa jumla maandishi katika leso ni mapambo ya leso. Iwapo leso haijaandikwa basi kwa Mswahili hiyo si leso.

**Kurekebisha**

Mwanamke Mswahili akitaka kumsuta jirani yake si lazima amkabili uso kwa uso. Atamtembelea nyumbani kwake huku kiunoni amejifunga leso yenye ujumbe wa kurekebisha kama huu: "Ukiona vyaelea vimeundwa". Maandishi katika leso pia hutoa maadili. Maadili haya ni kutumia maneno mazuri mtu anapoongea; kwamba uzuri wa mtu huonyeshwa kwa vitendo na mienendo yake na kadhalika. Kwa jumla, maneno yanayoandikwa katika leso huweza kueneza lugha ya Kiswahili pakubwa.

Enock Nyariki, *Taifa leo* (2015)

https://xtremepape.rs/

**Matini B**

# Nyota

Soma maelezo ya nyota zifuatazo. Tabiri maisha yako ya baadaye kwa kutumia siku yako ya kuzaliwa.

## Kondoo

**Machi 21–April 20**



Zungumza na mshirika wako wa karibu kuhusu kazi au biashara unayonuia kuifanya na utaona mafanikio yakikufuata. Umekosa kufanikiwa katika baadhi ya mambo kwa kutofuata ushauri.

## Ng'ombe

**April 21–Mei 20**



Roho yako nzuri kwa marafiki itakuletea manufaa hivi karibuni na waweza kujikuta umepanda ngazi katika shughuli zako. Usiache kutenda wema na kwenda zako.

## Mapacha

**Mei 21–Juni 21**



Utapokea ujumbe kutoka kwa mtu ambaye hamjaonana kwa muda mrefu na bila shaka utafurahi sana. Litakuwa funzo zuri kwako kuwa usitupe marafiki wa zamani kwani kila mtu ana heri yake.

## Kaa

**Juni 22–Julai 22**



Unajaribu kusahau makosa uliyowatendea wengine lakini unaonywa kuwa hutaweza kuondoa ubaya walionao dhidi yako. Jambo pekee la kufanya usahau ni kumwendea kila mmoja wao na kumwomba msamaha.

## Simba

**Julai 23–Agosti 22**



Unaonekana kuwa na haraka sana kutimiza jambo katika maisha yako lakini unashauriwa kuwa ukiendelea hivyo hutaenda mbali. Haraka haraka haina baraka. Nenda polepole na hatimaye utafika.

## Mashuke

**Agosti 23–Septemba 23**



Unatoa huduma muhimu kwa watu wengine kwa moyo mmoja na uaminifu lakini wanapozipokea hawaoni hivyo na badala yake wanahisi kama kwamba unafanya hayo kwa manufaa yako mwenyewe. Hilo lisikufanye ukate tama. Mungu atakulipa.

## Mizani

**Septemba 24–Oktoba 23**



Usipendelee kununua vitu vya anasa na ambavyo bei yake haikuruhusu. Hakikisha umeishi kulingana na kipato chako. Afya njema ndio kitu bora zaidi.

Sheikh Khabib, *Taifa Jumapili* (2015)



https://xtremepape.rs/

**Matini C**

# Gor Mahia yakamilisha ziara ya pwani kwa ushindi

Mabingwa wa soka nchini, Gor Mahia wakamilisha ziara yao Mkoani Pwani kwa kuishinda Mombasa Combined mabao 2–1 kwenye mechi kali iliyofanyika Jumapili. Katika pambano hilo lililochezewa uwanja wa Kaunti ya Mombasa, timu ya nyumbani ilianza kulivamia lango la Gor na katika dakika ya nne, Crispin Odula alipoteza nafasi nzuri ya kufunga bao baada ya kupokea pasi safi iliyotokana na ushirikiano baina ya Makame Salim na Robert Mambo.



Katika dakika ya tisa, Gor ilichukua uongozi kupitia frikiki ya Zacharia Taofic iliyotokana na Jerry Santos kufanyiwa madhambi. Ilikuwa kwenye dakika ya 20 ndipo Mombasa ilipoweka sawa mabao (1–1), mfungaji akiwa Mambo aliyefunga kwa kichwa. Mombasa ilipata nafasi nzuri ya sekunde 30 kabla ya kipenga cha mapumziko wakati Ali Boki aliwachenga wachezaji wawili na kupitisha mpira kwa Matano Harun ambaye aliupiga kiki lakini ikaokolewa na kipa wa Gor, Bonface Oluoch. Mchezo ulizidi ukali kwenye kipindi cha lala salama huku kila timu iking'ang'ania kupata bao la ushindi.

Kwenye dakika ya 66 baada ya mapambano langoni mwa Mombasa, Ali Abondo aliyeingia badala ya Ronald Omimo akafungia Gor bao la ushindi. Kocha wa Mombasa Combined Abdulnassir Kassim aliwapongeza vijana wake kwa kucheza mchezo mzuri na kuwa na matumaini watafanya vizuri zaidi kwenye mechi watakazocheza siku zinazokuja.

"Kila tunapocheza mechi vijana wangu wanazidi kupata uzoefu na mimi sina shaka wakati utafika kwetu kuzishinda timu kubwa za hapa nchini na nchi jirani," akasema Kassim ambaye hapo awali aliandaa kikosi hicho kwenda sare na Coastal Union ya Tanga mwezi uliopita. Kikoso hicho kiliimarishwa kutokana na kuwepo kwa aliyekuwa kiongozi wa Harambee Stars, Robert Mambo na Crispin Odulo ambaye alichezea Bandari msimu huu lakini haijafahamika mwaka huu atachezea kilabu gani.

Mwanasoka mwingine aliyevutia macho ya mashabiki ni Makame Salim ambaye huenda akachezea mojawapo ya timu za Nairobi kwenye supaligi ya Taifa ama ligi ya Taifa daraja la kwanza msimu huu wa 2015.

Abdulrahman Sheriff na Thomas Matiko, *Taifa Leo* (2015)

https://xtremepape.rs/

**Matini D**

JAMHURI
Tunaanzia Wanapoishia Wengine

# Wakati Dar kumejaa, tusisahau vijijini

Jiji la Dar es Salaam limejaa. Watu, magari, na changamoto za kila aina. Hesabu ya sensa ya Taifa ya mwaka 2012 ilionyesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na wakazi 3133 kwa kilomita moja na wastani wa Taifa ulikuwa watu 51 kwa kilomita moja. Mkoa wa Dar es Salaam ulikadiriwa kuwa na wakazi 4 360 000 na ndiyo unaoongoza kwa kuwa na wakazi wengi ukilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania. Ongezeka la watu jijini humu linatokana na uhamiaji wa watu kutoka vijijini.

Sababu kubwa ya msingi inayofanya watu kuhama vijijini ni kukosa kazi. Wahamiaji wengi ni vijana ambao huenda mijini kutafuta ajira. Shughuli kubwa ya vijijini ni kilimo, lakini vikwazo mbalimbali vinawafanya vijana kuamua kuwa ni bora kutafuta ajira za mijini kuliko kushiriki kwenye shughuli za kilimo. Kikwazo kingine ni kuwa bei za mazao mengi hazipandi kwa kasi inayolingana na kupanda kwa gharama za maisha, kwa hiyo kila miaka inavyozidi kusonga mbele, ndivyo mkulima anavyojikuta anakabiliwa na gharama ambazo hupanda.

Kuna sababu nyingine inayohamisha watu vijijini. Vijana wengi huhamia mijini kwa ajili ya kufuata elimu na wanapomaliza elimu zao hubaki mijini kwa sababu hawaoni fursa za kazi vijijini zinazolingana na elimu yao. Hapa yafaa kukumbuka aliyoyasisitiza Mwalimu Nyerere kwenye Sera ya Elimu ya kujitegemea kwamba ni muhimu elimu iwaandae wanafunzi kukabiliana na mahitaji na changamoto zilizopo kwenye maeneo wanaoyoishi.

Athari mojawapo kubwa ya ongezeko la watu jijini Dar es Salaam ni kuwa vijana wanaohamia jijini huwaacha wazazi vijijini ambao hawana nguvu ya kazi ambayo zamani iliwasaidia kumudu gharama za maisha. Matokeo yake ni kuwa utakuta baadhi ya wazee ambao wanahangaika na shughuli ambazo zingefanywa na watoto wao.

Tatizo lengine la kasi kubwa ya uhamiaji kuja Dar es Salaam ni ongezeko la makazi holela katika maeneo ambayo ni hatarishi kama vile mabonde ya mito. Mvua kubwa au za mfululizo zinaponyesha zinasababisha mafuriko yanayoleta pia hasara ya mali na hata kupoteza maisha.

Suluhisho linajulikana tangu zamani. Ni pale maendeleo ya kweli yatakapofika vijijini ndiyo watu wataacha kuhamia mijini. Kwa mara nyingi, imetamkwa na viongozi wengi kuwa kilimo ndiyo kazi ya msingi ya Watanzania walio wengi, na ni kwa kuendeleza kilimo kwa dhati ndiyo itawezekana kuongeza pato la Watanzania wengi na kupunguza kasi ya kuhamia mijini.

www.jamhurimedia.co.tz (2015)

https://xtremepape.rs/